


Kiswahili/Swahili

Ili kupata huduma zinazohitajiwa na jamii yetu kwa ajili ya uthabiti wa baadaye, lazima kwanza tuelewe sisi ni kina nani kama taifa. Hii ndiyo maana kuna sensa.

Sensa ni zoezi la kikatiba linalohitaji la kuhesabu wakaazi wote wa Marekani - walio raia au wasiokuwa raia. Takwimu itakayopatikana kupitia sensa husaidia serikali ya Marekani kutumia zaidi ya dola bilioni \$400 kuendesha shughuli za serikali kila mwaka kwa:

- *Hospitali*
- *Taasisi za mafunzo ya kazi*
- *Mashule*
- *Taasisi za elimu ya juu*
- *Madaraja, Mipenyo ya chini na miradi ya ujenzi miundombinu*
- *Huduma za dharura*



Sensa pia husaidia kukadiria idadi ya viti vya bunge vya Jimbo lenu kwenye Bunge la Waakilishi la serikali ya Marekani.

Hatutaweza Kuendelea Hadi Utakapotureshea.

Mnamo mwezi wa Machi 2010, fomu ndogo ya uhojaji yenye maswali kumi itawasilishwa kila nyumba kote nchini Marekani, na Puerto Rico. Utakapopokea fomu yako, jibu maswali yote 10 yaliyo mafupi kisha utume kwetu ukitumia bahasha iliyokwisha lipiwa gharama ya posta iliyo ambatanishwa.

Fomu ya sensa ni RAHISI KUJAZA, ni MUHIMU kwako na kwa hali ya baadaye ya jamii yako na ni SALAMA.

Hali yako na maelezo unayoyotoa yatalindwa na kuwekwa kwa siri chini ya sheria ya nchi. Pamoja na hayo, hutaulizwa juu ya haki yako ya kisheria ya ukaazi katika nchi hii.

Ikiwa hutairejesha fomu hiyo, basi huenda ukatembelwa na afisa wa sensa wa kuchukua fomu. Afisa wa kuchukua fomu za sensa ni mtumishi wa Halmashauri ya Serikali ya Marekani, mara nyingi atakuwa ni mtu kutoka kwa jamii yenu ambaye atatembelea makao yako kunakili habari zote zinazohitajika kwenye fomu ya sensa.

Kila Afisa Wa Sensa Amelishwa Kiapo Cha Kulinda Habari Zozote Utakazotoa. Hii Ni Sheria.

Tukikosa kupokea kidadisi kilichokamilishwa kwa barua pepe, mfanyikazi wa sensa atakuja nyumbani mwako ili kupata maelezo.

Chunguza Fomu Ya Sensa Ya 2010 Sasa

Anza mapema kujifahamisha juu ya sensa hii kwa kutumia Mwongozo wa Usaidizi wa Lugha. Mwongozo wa Usaidizi wa Lugha hupatikana kwa lugha 59 na utakusaidia kujaza fomu ya sensa kwa lugha ya Kiingereza.

[Nakili mwongozo kwa lugha yako sasa kwa kubonyeza hapa.](#)